# HALMASHAURI YA MANISPAA YA ILEMELA

*Mhe. Mwenyekiti na Wajumbe*

*Baraza la Madiwani,*

*Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela.*

*MWANZA*

***YAH: TAARIFA YA MKURUGENZI KATIKA MKUTANO WA BARAZA LA MADIWANI KWA ROBO YA NNE (APRILI–JUNI) TAREHE 29/08/2019 MWAKA WA FEDHA 2018/2019***

## 1.0. UTANGULIZI

***Mhe. Mwenyekiti***, Kwa mujibu wa Kanuni za kudumu za Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela za Mwaka 2014, Mkurugenzi anawajibika kulitaarifu Baraza la Madiwani kwa kutoa taarifa ya matukio mbalimbali ambayo yamefanyika au yanatarajia kutokea katika kipindi cha kila robo ya mwaka. Hivyo taarifa hii itagusa maeneo yafuatayo:-

i. Muhtasari wa Taarifa ya Mafanikio ya Utekelezaji wa Bajeti ya Halmashauri Kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019
ii. Taarifa ya ziara ya Katibu Mkuu wa CCM Dkt. Ally Bashiru
iii. Taarifa ya ziara ya Waziri wa Afya Mhe. Ummy Mwalimu
iv. Taarifa ya Lord Mayor kutoka Ujerumani

## A: MUHTASARI WA TAARIFA YA MAFANIKIO YA UTEKELEZAJI WA BAJETI YA HALMASHAURI KWA MWAKA WA FEDHA 2018/2019

### 1. UTANGULIZI

*Mhe Mwenyekiti,* Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2018/2019, Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela iliidhinishiwa bajeti ya kiasi cha Tsh. 73,355,471,234.00 kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli mbalimbali kwa ajili ya maendeleo ya wananchi wa Wilaya ya Ilemela ili kuweza kufikia malengo yaliyowekwa. Jedwali lifuatalo linaonyesha bajeti iliyotengwa, mapato na matumizi hadi kufikia tarehe 30/06/2019 wakati tunafunga mwaka wa fedha 2018/2019.

| NA | CHANZO CHA FEDHA | MAKISIO 2018/2019 | MAPATO HADI JUNI 30, 2019 | MATUMIZI HADI JUNI 30, 2019 | % MAPATO | % MATUMIZI |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Mapato ya ndani | 9,024,065,000 | 8,051,895,514 | 7,532,311,592 | 89 | 83 |
| 2 | Matumizi ya kawaida (OC) | 3,891,371,500 | 2,028,062,789 | 1,742,694,456 | 52 | 45 |
| 3 | Mishahara (PE) | 40,605,556,448 | 31,103,702,000 | 31,103,702,000 | 77 | 77 |
| 4 | Miradi ya maendeleo | 19,834,478,286 | 4,811,040,424 | 4,022,263,973 | 24 | 20 |
| | **JUMLA** | **73,355,471,234** | **45,994,700,727** | **44,400,972,021** | **63** | **61** |

## 2. MAFANIKIO YA UTEKELEZAJI WA BAJETI 2018/2019

### 2.1 UKUSANYAJI WA MAPATO NA USIMAMIZI WA FEDHA ZA UMMA,

- *Mhe Mwenyekiti,* Kuongeza kiwango cha mapato ghafi ya ndani yaliyokusanywa kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2018/2019 hadi kufikia Tsh. 8,051,895,514.00 sawa na asilimia 89 ya lengo ukilinganisha na kiwango cha mapato ya ndani kilichokusanywa mwaka wa fedha 2017/2018 kiasi cha Tsh. 4,689,593,341.75 ambapo ni sawa na ongezeko la asilimia 42. Hatua hii imetokana na kuimarika kwa mifumo ya kielektronic ya ukusanyaji wa mapato ya ndani pamoja na usimamizi madhubuti wa Halmashauri kwa usirikiano mzuri uliopo kati ya watendaji na Waheshimiwa Madiwani.
- Kusimamia vizuri matumizi ya fedha za umma hali iliyopelekea kupata hati safi ya ukaguzi wa CAG kwa hesabu za mwaka wa fedha 2017/2018 pamoja na kupunguza kwa kiasi kikubwa hoja za ukaguzi ukilinganisha na miaka ya nyuma.

### 2.2 UCHANGIAJI WA MIFUKO YA VIJANA, WANAWAKE NA WALEMAVU

- Kuongeza kiwango cha kuchangia mifuko ya vijana, wanawake na walemavu kutoka kiasi cha Tsh. 116,000,000.00 kilichotolewa mwaka wa fedha 2017/2018 hadi kiasi cha Tsh. 501,000,000.00 sawa na ongezeko la asilimia 77.

- Kuongezeka kwa idadi ya vikundi vya wajasiriamali kutoka vikundi 137 vilivyokuwepo mwaka wa fedha 2017/2018 hadi vikundi 181 kwa mwaka wa fedha 2018/2019 hatua ambayo inaakisi maendeleo ya jamii kujinasua na wimbi la umasikini kupitia shughuli za kujiongezea kipato zinazoendeshwa na vikundi hivyo.

**2.3UTAWALA BORA**

- *Mhe Mwenyekiti,* Kuongezeka kwa tija ya utendaji kazi wa watumishi wa umma na uwajibikaji mzuri wa Waheshimiwa madiwani katika Halmashauri kutokana na usimamizi mzuri wa stahiki zao na uboreshaji wa mazingira ya kazi.
- Kupungua kwa kero za wananchi katika sekta mbalimbali hususani sekta ya ardhi pamoja na kupungua kwa malalamiko ya watumishi kutopata stahiki zao za kiutumishi.
- Kuongezeka kwa ufanisi wa uendeshaji wa vikao vya kisheria kulinganisha na miaka ya nyuma hatua ambayo imepelekea waheshimiwa Madiwani kuweza kusimamia vizuri utekelezaji wa shughuli za Halmashauri.
- Ujenzi wa kituo cha Polisi Buswelu na Nyamhongolo, hatua inayosogeza zaidi huduma za usalama wa raia na mali zao katika jamii.
- Kumaliza mgogoro wa ardhi wa muda mrefu wa eneo la jeshini ambapo Halmashauri ilipokea kiasi cha Tsh. 3,534,295,166.00 kutoka Serikali Kuu kwa ajili ya kulipa fidia wananchi 369 na hadi tarehe 23/08/2019 jumla ya wananchi 353 walikuwa wamelipwa, wananchi 6

malipo yalikuwa yanashughulikiwa na wananchi 10 walikuwa bado kuleta taarifa zao za benki. Jambo hili limefanikiwa kutokana na juhudi kubwa za Mheshimiwa Mbunge Dkt. Angeline Mabula.

- Halmashauri imepandisha madaraja watumishi 1,091 katika kada mbalimbali ambapo walimu walikuwa ni 790, watumishi wa afya 121 kada nyingine(Utawala) watumishi 178. Mpaka sasa ni watumishi 63 ambao wamerekebishiwa mishahara yao. Aidha, halmashauri imefanikiwa kusafisha taarifa za watumishi 3,224 ambao wapo katika mfumo Lawson.

## 2.4MIRADI YA MAENDELEO

- *Mhe Mwenyekiti,* Kufungua shule za msingi mpya 3 ambazo ni Ihalalo, Bezi na Kayenze Ndogo na kufanya ongezeko la idadi ya shule za msingi kutoka shule 73 mwaka wa fedha 2017/2018 hadi shule 76 mwaka wa fedha 2018/2019.

- Kufungua shule za sekondari mpya 3 ambazo ni Kayenze, Kisundi na Angeline Mabula na kufanya ongezeko la shule za sekondari kutoka 24 mwaka wa fedha 2017/2018 hadi shule 27 mwaka wa fedha 2018/2019.

- Kuanzisha kidato cha 5 katika shule ya sekondari Buswelu ambapo tayari idadi ya wanafunzi 28 wa kidato cha 5 wanaendelea na masomo katika mchepuo (combination) wa PGM na PCB.

- Kuongezeka kwa kiwango cha ufaulu wa wanafunzi wa darasa la saba kutoka asilimia 87.5 mwaka wa fedha 2017/2018 hadi asilimia 94.8 mwaka wa fedha 2018/2019. Aidha, Halmashauri ilishika nafasi

ya kwanza kimkoa na nafasi ya sita kitaifa katika mtihani wa darasa la saba wa mwaka 2018 ikilinganishwa na nafasi ya pili kimkoa na nafasi ya 20 kitaifa kwa mtihani wa mwaka 2017.

- Kuongezeka kwa kiwango cha ufaulu wa wanafunzi wa kidato cha nne kutoka asilimia 82.92 mwaka wa fedha 2017/2018 hadi asilimia 85.41 mwaka wa fedha 2018/2019. Aidha, Halmashauri ilishika nafasi ya kwanza kimkoa na nafasi ya 17 kitaifa katika mtihani wa kidato cha nne wa mwaka 2018 ikilinganishwa na nafasi ya pili kimkoa na nafasi ya 19 kitaifa kwa mtihani wa mwaka 2017.

- Kukamilisha ujenzi wa vyumba 25 vya madarasa katika shule za msingi na vyumba 36 vya madarasa katika shule za sekondari. Hatua hii imepelekea kufunguliwa kwa shule mpya 3 za msingi na shule mpya 3 za sekondari.

- Kuongezeka kwa kasi ya ujenzi wa maboma ya vyumba vya madarasa katika shule za msingi na sekondari hali iliyochangiwa kwa kiasi kikubwa na mradi wa matofali unaosimamiwa na Mheshimiwa Mbunge wa jimbo la Ilemela Dkt. Angeline Mabula pamoja na nguvu mpya za michango ya wananchi kwenye ujenzi wa miundombinu ya shule ambapo hadi tunafunga mwaka wa fedha 2018/2019 jumla ya Tsh. 210,000,000.00 za michango ya jamii zilikuwa zimekusanywa kwa mfumo mpya wa kielektronic uliotengenezwa na kitengo cha Tehama.

- Kufungua zahanati mpya moja ambayo ni Lukobe na kufanya ongezeko la zahanati kuwa 14 na vituo vya afya 3 kutoka zahanati 13 na vituo vya afya 3 mwaka wa fedha 2017/2018.

- Kuongezeka kwa idadi kubwa ya wagongwa na akina mama wanaojifungulia kwenye vituo vya Serikali vya huduma ya afya kutokana na uboreshaji mkubwa wa huduma za afya katika Wilaya hatua inayochangiwa na uboreshaji mkubwa wa miundombinu ya afya ikiwemo ujenzi na ukarabati mkubwa wa vituo vya afya Karume, Buzuruga na Sangabuye.
- Kufikia hatua ya mwisho ya ujenzi wa hospitali ya Wilaya katika eneo la Isanzu ambapo hadi sasa bado masuala ya umaliziaji wa mwisho ili hospitali iweze kuanza kutoa huduma za afya kwa wananchi wa Wilaya ya Ilemela.
- Kuanza kwa utekelezaji wa mradi mkubwa wa kimkakati wa ujenzi wa stendi ya mabasi na maegesho ya malori katika kata ya Nyamhongolo ambapo mkandarasi tayari amepatikana na amekabidhiwa eneo la ujenzi wa mradi huo. Mradi huo utaongeza kiasi kikubwa cha mapato ya Halmashauri na hatimaye kupanua wigo wa kujitegemea.
- Kuongezeka kwa mtandao wa barabara za lami kutoka kilomita 24 mwaka 2017/2018 hadi kilomita 36 mwaka 2018/2019. Hatua hii imetokana na usimamizi mzuri wa miradi ya TSCP ambapo wafadhili wamekuwa wakiridhika na kuendelea kutoa fedha kila mwaka. Mpango ujao ni kujenga kwa kiwango cha lami barabara za Kahama – Kabusungu – Kayenze, Mbogamboga – Nyamadoke – Nyamhongolo, Buswelu – Cocacola na Pasiansi – Lumala – Kiseke. Tayari maandiko ya miradi hiyo yanaendelea kufanyiwa kazi na mradi wa TSCP.

- Kuongezeka kwa maeneo ya ardhi yaliyopangwa kimipangomiji ambapo hatua hii imetokana na juhudi za Mheshimiwa Mbunge Dkt. Angeline Mabula kusaidia upatikanaji wa fedha kiasi cha Tsh. 1,550,000,000.00 kutoka Serikali Kuu kwa ajili ya mradi wa upimaji viwanja. Mradi huu unatekelezwa katika eneo la East Buswelu ambapo viwanja 1200 vitauzwa na makisio ya mapato ya mradi huu ni Tsh. 5,537,984,000.00 hatua ambayo itaongeza mapato ya ndani ya Halmashauri kwa kiwango kikubwa.
- Kuongezeka kwa upatikanaji wa maji safi na salama kwa wananchi kutoka asilimia 30 mwaka wa fedha 2017/2018 hadi asilimia 45 mwaka wa fedha 2018/2019. Hatua hii imetokana na kuongezeka kwa mtandao wa usambazaji wa maji safi na salama kutoka katika miradi ya Igombe na Sangabuye.

## 3. CHANGAMOTO ZA UTEKELEZAJI WA BAJETI 2018/2019

- *Mhe Mwenyekiti,* Upungufu wa vitendea kazi hususani magari hali inayopelekea baadhi ya shughuli kukosa ufuatiliaji wa karibu
- Upungufu wa watumishi hususani watumishi wa Idara ya Ujenzi hali inayosababishwa baadhi ya miradi kukosa usimamizi mzuri wa kitaalamu kutoka kwa wataalam wa ujenzi.
- Kutopokelewa kwa fedha kutoka Serikali Kuu hatua ambayo inaathiri baadhi ya shughuli zilizopangwa kwa bajeti ya mapato ya ndani.

- Kutokea kwa shughuli nje ya bajeti zinazotokana na maelekezo yanayotokea wakati wa utekelezaji wa bajeti hali inayoathiri utekelezaji wa shughuli zilizopangwa katika bajeti husika.

**B: TAARIFA YA ZIARA YA KATIBU MKUU WA CCM DKT. ALLY BASHIRU**

***Mheshimiwa Mwenyekiti,*** Mnamo tarehe 30/07/2019 Katibu Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi(CCM) DKT. Ally Bashiru alitembelea Wilaya yetu ambapo alipata nafasi ya kupokea taarifa ya utekelezaji wa Ilani ya Chama Cha Mapinduzi kutoka kwa Mbunge wa Jimbo la Ilemela DKT. Angelina Mabula juu ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo na shughuli zingine za kijamii. Aidha Katibu Mkuu wa CCM aliipokea na kuipongeza taarifa hiyo namna ilivyoosheni shughuli mbalimbali za maendeleo na kwa jinsi ilivyotiza azima na matakwa ya Chama Cha Mapinduzi. Pia alieleza inaonesha ni namna gani palivyo na ushirikiano kati ya Wananchi, Mbunge na Watendaji wa Halmashauri ya Ilemela na kusisitiza kuendelea kudumisha ushirikiano huo ili kuwaletea wananchi wa Ilemela Maendeleo.

**C: TAARIFA YA ZIARA YA WAZIRI WA AFYA MHE. UMMY MWALIMU**

***Mheshimiwa Mwenyekiti,*** Mnamo tarehe 15/06/2019 Waziri wa Afya Maendeleo ya Jamii Jinsia Wazee na Watoto Mhe. Ummy A. Mwalimu alitembelea Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela na kufanya ufunguzi wa Mradi wa Ujenzi wa Jengo la Ebola Treatment Centre(ETC) kwa madhumuni ya kupokelea na kuhudumia wagonjwa/washukiwa wa magonjwa hatarishi ya Mlipuko kama vile Ebola Mafua ya Ndege na magonjwa mengineyo ya mlipuko, lililojengwa katika Halmashauri ya

Manispaa ya Ilemela kwa ajili ya walengwa wa Kanda ya Ziwa. Aidha aliwapongeza watumishi wa kila kitengo namna walivyojipanga kutoa taarifa za mshukiwa mgonjwa wa Ebora mara tu zinapojitokeza katika jamii, hadi huduma ya mgonjwa huyo inavyotolewa kwa mgonjwa na utolewaji wa taarifa katika Nyanja mbalimbali. Pia alielekeza kuwa katika Mashine ya upimaji wa virus vya Ebola inayotembea (Mobile Machine) moja wapo ipelekwe katika Hospitali ya Bugando kwa ajili ya eneo hili la Kanda ya ziwa.

## D: TAARIFA YA LORD MAYOR KUTOKA UJERUMANI

***Mhe Mwenyekiti***, Mnamo tarehe 12 -13/06/2019 Mstahiki Meya na viongozi wengine 3 wa kisiasa kutoka katika mji wa Wurzburg walitembelea katika Manispaa ya Ilemela na kujionea miradi mbalimbali inayosimamiwa na Schisto na kuonana na timu ya mradi, uongozi wa Mkoa na Madaktari wa Wilaya, Manispaa na Jiji; na kufanya majadiliano kwa lengo la kuimarisha miradi hiyo miwili. Aidha, wageni hao walitembelea kituo cha afya cha Karume watabibu na wateknolojia wa maabara na kuona darubini waliyofadhili. Kadhalika Wageni hao walitembelea shule ya Msingi moja wapo Kabangaja ambayo shughuli zake zilikuwa zinatekelezwa na CHAST intervation na kukutanana walimu 2 na wanafunzi 30 wanaoshiriki katika shughuli za CHAST.

Siku hiyo pia walikutana na wazee ambao wako katika mazingira magumu wanaoiwakilisha jamii (Viongozi wa mtaa, Viongozi wa BUM na Community drug distributors) katika kata ya Bugogwa na kufanya majadiliano ya kuimarisha huduma ya Kichocho ambapo jamii iliomba upatikanaji wa

chanzo cha maji safi na salama mbadala badala ya kutegenemea maji ya ziwa yaliyo chafuliwa (contaminated). Kwa ujumla wageni hawa aliahidi kutoa msaada zaidi kwa hatua nyingine za mradi, kuchimba kisima katika shule ya msingi Kabanganja na baadhi maeneo mengine ya mitaa hiyo.

Naomba kuwasilisha.

Daniel L. Batare

Kaimu Mkurugenzi wa Manispaa

**HALMASHAURI YA MANISPAA YA ILEMELA**